

# Alfond Grant ni nini?



Alfond Grant ni ruzuku wa \$500 uliowekezwa kwa ajili ya watoto wa Maine kwa kusudio la elimu yao baada ya shule ya upili. Msaada huu ni njia kuu ya kusaidia familia zinapoanza kujitayarisha, katika ule mwanzo kabisa wa maisha ya mtoto, kwa elimu ya juu zaidi. Ni zawadi kwa watoto wa Maine kutoka kwa mfanyibiashara wa Maine na mfadhili Harold Alfond.

**Nani anayestahili kupata Alfond Grant?** Kwanzia 2013, watoto wote waliozaliwa na wakazi wa Maine wanapewa ruzuku wa Alfond ya \$500. Kufikia mwanzoni mwa 2022, Msingi wa Udhadini wa Alfond Scholarship Foundation imewezeza zaidi ya \$64 milioni kwa zaidi ya watoto 128,000 wa Maine. Je, mtoto wako ni mmoja wao? Ruzuku wa Alfond ulipatikana kua msingi mdogo zaidi kuanzia 2008-2012. Tembelea [www.MyAlfondGrant.org](http://www.MyAlfondGrant.org) ili kujifunza zaidi.

## Msaada inatumika namuna ngani?

- Alfond Scholarship Foundation (ASF) unawezeza ruzuku wa Alfond wa \$500 kwa watoto wote wa Maine wanaostahili.
- Fedha hizo zinawekezwa katika akaunti zinazomilikiwa na Alfond Scholarship Foundation. Kwa sababu ya Msaada wa Alfond wa \$500 unawekezwa kwa mtoto aliye na umri mchanga, unao angaa miaka 18 ya kuwa na uwezo wa kukua.
- Ruzuku wa Alfond unaweza kutumika kwa karo ya shule vyaoni na vya vikuu, vya jumua na ajira nyingi au shule za biashara. Msaada huu unaweza pia kutumika kwa ajili ya makazi na malazi, vitabu na kompyuta.
- Familia zinapotaka kutoa michango yao wenyewe, zitahitaji kufungua akaunti zao wenyewe. NextGen 529® ni mpango wa 529 wa Maine, ambao familia nyingi zinatumia kuweka akiba kwa masomo ya baada ya shule ya upili. Ili kujifunza zaidi au kufungua akaunti yako mwenyewe, tembelea [NextGenforME.com](http://NextGenforME.com).

## Je, wazazi wanaweza kufanya nini?

Tovuti ya MyAlfondGrant inatoa maelezo, vidokezi na rasilimali kwa watoto na wazazi.

Tembelea tovuti yetu, [www.MyAlfondGrant.org](http://www.MyAlfondGrant.org), ili:

- Kuangalia thamani ya mtoto wako - thamani hii inabadilika baada ya muda!
- Kusasisha maelezo yako binafsi
- Kuunda MyPlan ili kusaidia mtoto wako kufaulu
- Kushiriki hadithi yako kuhusu familia yako au mtoto wako
- Kupata maelezo ili kumsaidia mtoto wako kwenye njia yao ya baadaye njema

  Tufuate kwenye Facebook na Instagram!

Alfond Scholarship Foundation si msambazaji aliyeidhinishwa wa NextGen 529.

*my*Alfond *grant*

ASF ni shirika linalojitegemea la 501(c)(3) lisilo la faida na halihusiani na au kutenda kazi chini ya mamlaka yoyote ya FAME. FAME haijaidhinisha mawasiliano ya ASF kwa ujumla, au nyenzo hizi haswa, na haiwajibikii maudhui ya mawasiliano yoyote ya ASF. Kuanzisha akaunti ya NextGen na kushiriki katika mpango wa 529 wa Maine lazima kupangwa kupitia maombi ya moja kwa moja kwa FAME. ASF haina mamlaka yoyote kutoka kwa FAME kutoa ofa yoyote, au kutoa mapendekezo au ushauri wowote, kuhusu kushiriki katika programu ya NextGen. NextGen 529 ni mpango wa Sehemu ya 529 unaosimamiwa na Mamlaka ya Fedha ya Maine (FAME, Finance Authority of Maine). Unaweza kupata Maelezo ya Programu ya NextGen 529 kwa kuomba nakala kutoka kwa mtaalamu wako wa fedha, kutembelea NextGenforME.com au kumpigia simu msimamizi wa programu kwa 1-833-336-4529. Maelezo ya Programu yana taarifa kamili zaidi, ikijumuisha malengo ya uwekezaji, malipo, gharama na hatari za kuwekeza kwenye NextGen 529, ambayo unapaswa kuzingatia kwa makini kabla ya kuwekeza. Akaunti za NextGen 529 si amana za benki na hazijawekewa bima na Shirika la Bima ya Amana ya Shirikisho (FDIC, Federal Deposit Insurance Corporation). Marejesho ya uwekezaji katika akaunti ya NextGen 529 hayajahakikishiwa au kuwekewa bima na Jimbo la Maine, FAME au watoa huduma wowote wa NextGen 529. Washiriki wa NextGen 529 watachukua hatari zote za uwekezaji katika akaunti za NextGen 529, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa hasara ya kupoteza amana na dhima ya adhabu za ushuru ambazo zinaweza kutathminiwa kulingana na uondoaji wa kiasi fulani kilichowekezwa katika NextGen 529. Ingawa ASF inaamini kwamba kuweka akiba na kuwekeza kwa ajili ya chuo kunawanufaisha watoto wa Maine, ASF inabainisha kuwa uwekezaji katika mipango ya 529 unaweza kupungua thamani kutokana na mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na maamuzi ya kimsingi ya uwekezaji na/ au vitendo vya au kutokufanya mambo fulani kwa watoa huduma. ASF haidai dhima yoyote ya marejesho ya mapato ya uwekezaji ya ruzuku ya mtoto ya Alfond au mchango wowote wa 529.